



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA JIMBO LA AMANI
NA KATA KUMI NA MBILI (12)

Dar es salaam, 30 Oktoba, 2022

1. Tume imepokea barua kutoka kwa Mhe. Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye Kumb. Na. CEA.137/400/14 ya tarehe 19 Oktoba, 2022 akiitaarifu Tume kuhusu kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Amani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Tanzania Zanzibar. Nafasi hiyo wazi imetokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mheshimiwa **Mussa Hassan Mussa** (CCM) kilichotokea tarehe 13 Oktoba, 2022. Taarifa hiyo ya Spika ni kwa mujibu wa kifungu cha 37 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Vilevile, Tume imepokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yenye Kumb. Na. CCB.126/443/01 ya tarehe 12 Septemba, 2022 akiitaarifu Tume juu ya uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika kata kumi na mbili (12) zilizoko kwenye halmashauri kumi na moja (11) za Tanzania Bara. Nafasi hizo zimetokana na vifo na kujiuzulu. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri ni kwa mujibu wa kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

2. RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE NA UDIWANI:

Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu 37 (1) (b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 13 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume imeandaa Uchaguzi Mdogo ili kujaza nafasi ya Ubunge Jimbo la Amani na nafasi za Udiwani kwenye Kata kumi na mbili (12) za Tanzania Bara.


Ratiba ya Uchaguzi mdogo katika Jimbo la Amani na Kata 12 ni kama ifuatavyo:

NA.	TUKIO	TAREHE
1.	Kutoa fomu za uteuzi	24 hadi 30 Novemba, 2022
2.	Uteuzi wa wagombea	30 Novemba, 2022
3.	Kampeni za uchaguzi	01 hadi 16 Disemba, 2022
4.	Siku ya kupiga kura	17 Disemba, 2022

KATA KUMI NA MBILI (12) ZA TANZANIA BARA ZITAKAZOSHIRIKI UCHAGUZI MDOGO NI:-

Na.	MKOA	HALMASHAURI	JIMBO	KATA
1.	Dar es Salaam	Jiji la Dar es Salaam	Ukonga	Majohe
2.	Dodoma	Wilaya ya Chamwino	Chamwino	Dabalo
3.	Mbeya	Wilaya ya Kyela	Kyela	Ibanda
4.	Mtwara	Wilaya ya Tandahimba	Tandahimba	Mndumbwe
5.	Njombe	Mji wa Njombe	Njombe Mjini	Njombe Mjini
6.	Pwani	Mji wa Kibaha	Kibaha Mjini	Misugusugu
		Wilaya ya Bagamoyo	Bagamoyo	Dunda
7.	Rukwa	Wilaya ya Sumbawanga	Kwela	Kalumbeleza
8.	Shinyanga	Manispaa ya Shinyanga	Shinyanga Mjini	Mwamalili
9.	Tanga	Jiji laTanga	Tanga Mjini	Mnyanjani
		Wilaya ya Lushoto	Mlalo	Lukozi
		Mji wa Handeni	Handeni Mjini	Vibaoni

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inavikumbusha vyama vya siasa pamoja na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo yatakayotolewa na Tume katika kipindi chote cha uchaguzi huo mdogo.


 Dkt. Wilson M. Charles
MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI